**OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

# HOTUBA

**YA**

**MHE. HAMZA SAIDI JOHARI**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI NA MWENYEKITI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KATIKA BARAZA LA WAFANYAKAZI**

**UKUMBI WA MIKUTANO WA MABEYO - DODOMA**

**18 AGOSTI, 2025**

- **Bw. Samwel Marco Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Bi. Faith Minani, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu;**
- **Bw. Hassan Nkya, Katibu Msaidizi wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**
- **Bi. Zella Kiliat Lwemanyila, Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Bi. Beatrice Jeremiah Nzobanaliba, Katibu wa TUGHE, Tawi la Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**
- **Mwakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi,**
- **Mwakilishi wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini;**
- **Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Wageni Waalikwa;**
- **Mabibi na Mabwana;**

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**Watumishi wenzangu na wajumbe wa Baraza;**

Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, afya na fursa ya kuweza kukutana hapa siku ya leo katika Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Ninawashukuru wajumbe wa Baraza, wageni waalikwa kwa kutenga muda wenu kuja kuungana nasi katika siku hii. Aidha, nitakuwa mchoyo wa fadhila, kama sitawashukuru wajumbe wa Sekretarieti na wote waliohusika kuandaa Mkutano huu. Ninatambua kila mmoja wetu ana majukumu mazito lakini kwa kutambua umuhimu wa mkutano huu, mmeacha shughuli zenu ili muweze kujumuika nasi hapa siku ya leo. Hongereni sana.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Kama mnavyofahamu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzishwa chini ya Ibara ya 59 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kupewa jukumu la kuishauri Serikali kuhusu mambo yote ya kisheria ndani na nje ya nchi. Ofisi inatekeleza majukumu haya kupitia Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 pamoja na sheria mbalimbali za kazi, kama vile, Agizo la Rais Na. 1 la mwaka 1970, Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2003, Sheria ya

Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 na Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105.

Kwa mujibu wa sheria hizo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama ilivyo kwa Taasisi zingine za Umma, inapaswa kuwashirikisha wafanyakazi wake katika masuala mbalimbali yanayohusu maslahi ya watumishi ikiwemo uandaaji na utekelezaji wa mpango na bajeti na kujadili hoja mbalimbali zinazotokana na utekelezaji wa mpango na bajeti ili kuzishauri menejimenti ipasavyo. Aidha, kwa mujibu wa ibara ya 13.1 (c) ya Mkataba wa kuunda Baraza la Wafanyakazi kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na TUGHE wa mwaka 2020, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inapaswa kufanya Mikutano ya Baraza la Wafanyakazi si chini ya mara mbili kwa mwaka. Napenda kuwafahamisha kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatekeleza suala hili kikamilifu ambapo Mkutano wa mwisho kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ulifanyika katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere Kibaha, Pwani tarehe 24 Januari, 2025 kwa lengo la kupokea na kujadili taarifa ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mwaka wa Fedha 2025/2026. Mkutano huu ni mkutano wa kwanza kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Ajenda za Mkutano huu ni; kupokea taarifa ya utekelezaji wa kazi za TUGHE Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hotuba ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Baraza, kupitia muhtasari wa yatokanayo na kikao cha Baraza kilichofanyika tarehe 24 Januari, 2025, kupokea taarifa ya mpango na bajeti ya mwaka 2025/2026 na wasilisho la

mpango wa mafunzo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na mapendekezo ya mafunzo kwa mwaka 2026/2027 – 2032.

Ajenda ya kupokea na kujadili Taarifa ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 ikiwa ndio ajenda kuu, baada ya Mkutano huu kufunguliwa rasmi, wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali watapata fursa ya kupokea na kujadili hoja mbalimbali zitakazoibuliwa katika taarifa hizo na kisha kutoa mapendekezo mbalimbali ambayo yatawasilishwa kwa mamlaka husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Baada ya maelezo hayo, ninapenda pia kuwajulisha kuwa, katika Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 ulioishia mwezi Juni, 2025, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanikiwa kutekeleza Mpango Kazi wake kama ifuatavyo:

i. Ofisi iliandaa Miswada mbalimbali ya Sheria 19,
ii. Sheria Kuu 433 zilitafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili,
iii. Maazimio mawili (2) yaliandaliwa na kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
iv. Ofisi ilikamilisha Urekebu wa Sheria Kuu 446 za nchi na kuandaa Toleo la Sheria zilizofanyiwa Urekebu la Mwaka 2023,
v. Ofisi ilifanya upekuzi wa jumla ya Mikataba 3,436 ya Kitaifa na Kimataifa. Mikataba hii ambayo ilitoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilihusisha masuala ya ununuzi, ujenzi, ukarabati wa majengo na utoaji huduma za jamii,

vi. Hati za Makubaliano (Memoranda of Understanding) 729 zilifanyiwa upekuzi,

vii. Maombi ya ushauri wa kisheria 4,151 yalipokelewa na kufanyiwa kazi,

viii. Ofisi iliendelea kuboresha huduma kwa watumishi kwa kulipa motisha kwa watumishi kuanzia mwezi Januari, 2025,

ix. Ofisi iliandaa na kuwezesha kikao kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kilichofanyika tarehe 03 Desemba, 2024 katika Mkoa wa Dodoma,

x. Kuendesha, kusimamia na kushiriki katika majadiliano yahusuyo mikataba na usuluhishi wa mashauri ya madai,

xi. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utendaji kazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

xii. Kushiriki katika vikao vya Kikanda na Kimataifa ambavyo Serikali ina maslahi,

xiii. Kuratibu na kufanikisha shughuli za utoaji wa ushauri wa kisheria kupitia Kliniki katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Kilimanjaro na Singida,

xiv. Kuanzisha na kuzindua Kamati za Ushauri za Mikoa ya Mwanza, Dodoma, Kilimanjaro na Singida,

xv. Ofisi imewezesha Watumishi kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika fani mbalimbali ndani na nje ya Nchi,

xvi. Kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria ambako kumeiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu na kukidhi mahitaji ya nchi yetu,

xvii. Ofisi imeendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Majengo ya Vituo Jumuishi katika mikoa ya Mwanza na Arusha pamoja na Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Jijini Dodoma,

xviii. Ofisi imeajiri watumishi wapya 17 na imepokea watumishi 21 kwa njia ya uhamisho.

xix. Ofisi imenunua vifaa vya mbalimbali vya Tehama na shajala.

xx. Kuratibu na kuwezesha mafunzo kwa Mawakili wa Serikali wote yaliyofanyika Arusha ”Bespoke”.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Wakati tukiendelea kutekeleza mipango ili kufikia malengo yetu, natambua kuwa bado zipo changamoto kadhaa ambazo bado zinaendelea kupatiwa ufumbuzi. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na;

i. Uhitaji wa rasilimali watu,

ii. Upungufu wa vitendea kazi ikiwemo magari na vifaa vya TEHAMA,

iii. Maslahi ya watumishi kama vile uboreshaji wa mishahara na

iv. Ufinyu wa nafasi za Ofisi.

Hata hivyo, pamoja na changamoto hizo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutekeleza mpango kazi wake wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Ni vyema tufahamishane kuwa, tunapoendelea kutekeleza majukumu yetu, changamoto haziwezi kukosekana au kwisha kabisa, hivyo kwa rasilimali tulizonazo, niwaombe tuendelee kutekeleza majukumu yetu kwa weledi, uadilifu, umakini na uaminifu. Kwa upande wangu na kwa niaba ya Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, niahidi kuwa tutazidi kuzipatia ufumbuzi changamoto husika kwa kadri ambavyo uwezo wa Ofisi utakavyoruhusu.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Wakati nikielekea kuhitimisha Hotuba yangu, naomba nitumie nafasi hii kuwakumbusha wajumbe wa Baraza waliopo hapa ambao ni wawakilishi wa watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuzingatia masuala yafuatayo:

Dira ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaongozwa na Dira na Dhima zifuatazo:

***Dira:*** *Kuwa Taasisi yenye ufanisi, kitaaluma na kuaminika katika kutoa huduma bora za kisheria kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

***Dhima:*** *Kutoa Huduma za Kisheria zenye ubora kwa njia ya kuandaa Sheria, Upekuzi na Majadiliano ya Mikataba pamoja na Ushauri wa Kisheria kwa maendeleo ya Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa.*

Ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika Dira na Dhima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanapaswa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma na misingi mikuu minne ambayo ni **utaalamu/weledi, ubunifu, uadilifu na uwazi.** Misingi hii, pamoja na mambo mengine, pia inatulazimu watumishi wote wa umma kuzingatia yafuatayo;

i. **Utunzaji wa siri za Serikali**

Hivi karibuni, kumeibuka tabia ya watumishi kuvujisha siri za Ofisi huku wakifahamu fika kuwa, kufanya hivi ni kinyume na Miongozo, Kanuni na Sheria za Nchi. Kwa Hotuba hii, niwatake watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha hawatoi nyaraka au taarifa yeyote ile ya Ofisi kwa mtu yeyote asiyehusika au bila idhini/kibali kutoka kwa mwenye Mamlaka. Katika hili, kama ilivyo kwa mambo mengine ya utovu wa maadili, tutakuwa wakali na hatutasita kuchukua hatua za kisheria kwa yeyote atakayebainika kuvujisha siri za Ofisi/Serikali.

ii. Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali lina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kunakuwa na nidhamu ya kazi, maelewano, ushirikiano na mshikamano kati ya Wafanyakazi na Menejimenti ili kuleta tija na ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia, watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanapaswa kufahamu kwamba ni wajibu wetu kuheshimiana bila kujali tofauti zetu za kada na wadhifa tulionao. Hatua za kinidhamu zichukuliwe mara moja kwa watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria

Mkuu wa Serikali watakaobainika kuharibu taswira ya Ofisi yetu kwa kujihusisha na vitendo vilivyo kinyume na maadili ya utumishi wa umma kama vile uvaaji mbaya, tabia ya ulevi, uzembe, rushwa na udanganyifu. Katika hili, Kanuni zetu za Maadili dhidi ya mawakili wanaokiuka maadili katika utekelezaji wa majukumu yetu - "The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Provision of Legal Opinion by State Attorneys and Law Officers in Public Service) Guidelines, G.N 32/2023 zilizochapishwa tarehe 20 Januari, 2023 zitatumika ipasavyo.

iii. Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo kuhakikisha mnapitia na kujiridhisha na kazi zilizofanywa na maafisa ambao wapo chini yenu kabla kazi husika hazijatoka nje ya Ofisi. Vilvile Wakurugenzi na Wakuu wa vitengo mtengeneze utaratibu wa kuwatumia Maafisa wanadamizi ili kujengea uwezo maafisa wa chini na pia kuendelea kudumisha ueledi na ubora wa kazi zetu. Vivyo hivyo, maafisa wa ngazi za chini wajenge desturi ya kupitisha kazi zao kwa maafisa wenzao ili kuondoa dosari za kimaudhui na kiuandishi kwa kazi zinazotoka nje ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hivyo kuweka taswira nzuri ya Ofisi.

iv. Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuzidi kutafuta fursa za kuwaendeleza kielimu na kimafunzo watumishi ili kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na mbinu za kisasa za utendaji kazi. Napenda kutoa rai kwa watumishi wote kuwa, kila mmoja anapaswa, iwe kwa kujigharamia au

kugharamiwa na Serikali ahakikishe anapata mafunzo ya muda mfupi au hata ya mrefu kwa madhumuni ya kuendana na wakati. Kamwe tusibweteke.

v. Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tunapotoa huduma kwa wadau mbalimbali kwa niaba ya Serikali, tuhakikishe wateja wetu wanapata huduma hiyo kwa wakati kwa kuzingatia muda ulioainishwa katika Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa mwaka 2022. Utoaji wa huduma bora, uendane na matumizi ya lugha nzuri yenye staha.

vi. Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuongeze ushiriki katika kufanya mazoezi, mabonanza na michezo ya SHIMIWI, kwani michezo mbali ya kujenga na kuimarisha afya, umoja, uhusiano na ushirikiano lakini pia huboresha ufanisi katika maeneo yetu ya kazi.

Maafisa wote tulio hapa, ni jukumu letu kuhakikisha Dhima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatekelezwa ili kufikia Dira ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Mtakumbuka kuwa, mnamo tarehe 17 Julai, 2025, nchi yetu ilizindua rasmi Dira ya Maendeleo ya miaka 25, maarufu kama “Dira 2050”. Katika hotuba ya kuzindua Dira hiyo, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alibainisha kuwa, dira ni mpango jumuishi, uliobeba maono ya masafa marefu, yakiakisi matarajiio na matamanio ya Watanzania kwa kipindi cha miaka 25 ijayo.

Kwa mujibu wa Mheshimiwa Rais, ili kufikia dira ya kuwa Nchi ya Uchumi wa Kati Ngazi ya Juu unaoongozwa na maarifa na Uchumi wa viwanda, ni lazima kila mmoja kujenga na kudumisha utamaduni wa uwajibikaji unaozingatia weledi, ubunifu katika utekezaji wa majukumu yetu mbalimbali.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwa ni Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala yote ya kisheria, tunapaswa kuhakikisha kuwa, sheria, sera, mipango, malengo na mikakati mbalimbali pamoja na vigezo na viashiria vilivyowekwa vya upimaji wa matokeo ya kiutendaji wa Watumishi wa umma, vinafungamanishwa na malengo na shabaha ya Dira ya 2050.

Kadhalika, tunapaswa kubuni, kupanga na kutekeleza mifumo ya uwajibikaji na ufuatiliaji, upimaji na tathmini ya matokeo ya kazi zetu huku tukiongozwa na tunu za weledi, umakini, ufanisi na uwazi.

Ofisi yetu, inao wajibu wa kupanga, kuratibu, kutekeleza michakato ya tathimini na mapitio ya sheria za Bunge na sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizotungwa, zinazotungwa na zitakazotungwa kwa lengo la kufanya maboresho na marekebisho muhimu kwa minajili ya kuziwezesha Taasisi za Umma kushiriki kikamilifu na kwa tija katika utekelezaji wa Dira ya 2050 kwa ufanisi na tija.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Kama mnavyofahamu, mwaka huu Nchi yetu itakuwa na Uchaguzi Mkuu, ambapo wananchi watapata fursa ya kuchagua viongozi katika nafasi ya Udiwani, Ubunge na Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa Tume Huru ya Uchaguzi (INEC) nchini, Jumatano ya tarehe 29 Oktoba, 2025 imetangazwa kuwa siku ya uchaguzi mkuu nchini, hivyo kupitia adhara hii, nitoe wito kwa watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wananchi kwa ujumla, kushiriki kikamilifu katika mchakato wa uchaguzi kwa kufuatilia, kuelewa na kupima sera za wagombea na kisha kuchagua viongozi bora watakaotuongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Sisi tulio katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambao ni mkono muhimu wa kisheria kwa Serikali, tutambue kuwa kupiga kura na kuchagua viongozi wetu ni haki yetu ya msingi ya Kikatiba. Aidha, tukawe mabalozi kwa kuwaelimsha ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wengine juu ya umuhimu wa kupiga kura na kuchagua viongozi sahihi ambao wataendelea si tu kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Nchi yetu, bali watakao hakikisha tunu ya amani na utulivu zinadumishwa na kuendelezwa.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Katika Mkutano huu, pamoja na mambo mengine, wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali watapokea na kujadili Taarifa ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026. Naomba wajumbe wote tusikilize mawasilisho kwa makini, na wakati utakapofika tutoe michango yetu kwa uwazi ili baadae maazimio ya Mkutano huu yatumike kuboresha mpango kazi na bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2024/25.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Baada ya kusema hayo, kwa heshima na taadhima naomba sasa nitamke kuwa, Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali umefunguliwa rasmi.

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**

Hamza S. Johari

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKLI**